

## Class 5 mid term 1 2021

### Kiswahili

#### ZOEZI LA 1: KUSOMA KWA UFAHAMU.

Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.

Sungura na familia yake waliishi katika msitu mdogo wa Mbotela. Mara kwa mara, ilimbidi amtembelee rafiki yake, Kinyonga, ambaye aliishi katika msitu jirani wa Kitivo. Sungura alikuwa akimtembelea kwa sababu hakuwa na jirani yeyote. Kinyonga hakuweza kumtembelea Sungura kwa sababu hakuweza kutembea kwa kasi kama Sungura. Siku moja, Sungura aliwaambia watoto wake, "Leo, sote tutaenda kwa Kinyonga ili tukamsaidie maana ni mgonjwa na hawezi kufanya kazi za nyumboni." Watoto waliposikia hivyo, walifurahi na kurukaruka.

1. Ni familia ngapi zimetajwa katika hadithi hii? \_\_\_\_\_
2. Sungura na familia yake waliishi katika msitu gani? \_\_\_\_\_
3. Ni nani aliyeishi katika msitu wa Kitivo? \_\_\_\_\_
4. Je, ni kwa nini Kinyonga hakuweza kumtembelea Sungura? \_\_\_\_\_
5. Sungura na watoto wake wangeenda kwa Kinyonga kufanya nini?  
\_\_\_\_\_

Alama
5

#### ZOEZI LA 2: SARUFI

Chagua neno sahihi kujazia pingo.

barakoa	midomo	Korona	karantini	mikono
---------	--------	--------	-----------	--------

Bwana Kenge alipoingia darasani, alitueleza kuwa ugonjwa wa \_\_\_\_\_

bado uko na kwa hivyo tulitakiwa kunawa mikono kila mara na kuvalia \_\_\_\_\_

kuziba pua na \_\_\_\_\_. Alitukataza kukaribiana kupita kiasi na kusalimiana  
8

kwa \_\_\_\_\_. "Yeyote mwenye dalili za ugonjwa huu anapaswa kutengwa  
9

katika \_\_\_\_\_ hali yake inapozidi kuimarika," akaongeza.

10

Aina za nomino zilizopigiwa misitari ni za aina gani?

11. Shangazi yangu ataenda Nairobi.
12. Dawati la Maunda limevunjika.
13. Nilipohisi kiu niliyanywa maji.
14. Watoto wadogo hupenda kucheza pamoja.

Andika kwa umoja au wingi kwa usahihi.

15. Nyuki ametengeneza asali.
16. Milingoti ile imevunjika.
17. Pera hilo limeanguka.
18. Vyakula vimepikwa.

Andika sentensi upya ukitumia vinyume vya maneno yenyeye mistari.

19. Nilimwona mfalme akitangaza.
20. Bwana Kazamoyo ni mkulima maskini.
21. Wavulana wote wameenda uwanjani.

22. Ninapenda kusafiri usiku.

Andika sentensi hizi katika nyakati za mabanoni.

23. Mimi ninamwandikia kaka barua. (wakati ujao)

24. Ni nani ataniokotea kalamu yangu? (wakati uliopita)

25. Mbosso aliimba kwa sauti nyororo. (wakati uliopo)

26. Ukuta wa choo ulijengwa upya. (wakati ujao)

Andika ukubwa wa majina haya.

27. Mbwa
28. Mto
29. Mtu
30. Mti

Alama

### ZOEZI LA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amwamkue mwanafunzi na kumiwomba gkae. Mwalimu ajitambulisse.

"Mimi ni mwalimu \_\_\_\_\_ Niambie jina lako."

"Leo ningependa tuzungumze kuhusu mapishi."

1. Unga wa mahindi huweza kutumiwa kupikia nini?
2. Ni nini hutiwa katika chakula ili kuongeza ladha?
3. Chai hupikwaje?
4. Taja chakula kimoja kinachoweza kupikwa kwa unga wa ngano.
5. Taja chakula kimoja ambacho hukaangwa.

Alama
5

### ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI.

Wakulima ni watu muhimu sana katika jamii. Wao hukuza mimea na kuwafuga wanyama mbalimbali. Ni kweli kuwa, nyingi kati ya bidhaa ambazo hutumiwa hasa katika mapishi hutokana na shughuli za ukulima; maziwa, unga, sukari, mayai, nyama na kadhalika hutokana na bidii za wakulima. Watu wengine hawapendi-kazi hii ya ukulima kwa sababu wanaamini ni kazi duni na yenye uchafu mwingu. Inafaa wajue kuwa kazi ni kazi, mradi mkono uende kinywani.

Alama
10